BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

POMADE
YA MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

# Harambee Ya Msikiti Wa Shakombo Kufanyika Mnamo Novemba 10

na Abdulrahman Sheriff

HARAMBEE kubwa ya kuchangia ujenzi wa Msikiti wa Kisasa utakaogharimu kiasi cha Shilingi Milioni Nane Unusu (8.500.000/-) itafanyika katika sehemu ya Mtongwe Vijiweni iliyoko katika Mombasa Kusini mnamo Novemba 10, mwaka huu.

Mwanzilishi wa mpango wa majenzi ya Msikiti huo unaojulikana kama *"Shakombo Masjid"*, Bw. Khamis Ramadhan Mwadzengo aliliambia *Coastweek* kuwa mkutano huo wa Harambee utafanyika kwenye sehemu hiyo ya Msikiti ambao umeshaanza kujengwa.

Majenzi ya msikiti huo yalianza toka mwaka 1981 na Bw. Mwadzengo akawa na matumaini kwamba Waislamu watajitokeza kwa wingi na kuchangia mpango huo ili upate kukamilishwa. Katika Msikiti huo, pia kutakua na Madrassa ya kufundishia watoto Qur'ani na Masomo ya Dini ya Kiislamu.

Bw. Mwadzengo alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Pwani Bw. Yusuf Mohammed Haji kwa kukubali kwake kuhudhuria kwenye Harambee hiyo. Alisema Mgeni wa Heshima atakuwa Waziri Mdogo wa Ardhi na Makao, Sheriff Nassir aliye pia Mwenyekiti wa Kanu wilayani Mombasa.

Mwanzilishi huyo alitoa ombi kwa Waislamu na wananchi wote kujitolea kwa mioyo mikunjufu kuchangia Msikiti huo kwani alisema, *"Wanaopenda kheri basi hii ni njia mojawapo ya kujipatia Thawabu. Kila la kheri liwafikie wote watakaosaidia mpango huu wa majenzi wa nyumba ya Mwenye-Ezi-Mungu".*

**Akitoa historia fupi ya msikiti huo, Bw. Mwadzengo alisema kuwa ulijengwa miaka 39 iliyopita ukijulikana kama Misikiti wa Almarhum Shakombo Bin Mwaurinda. "Tumefikiria kuujenga upya na wa kisasa kutokana na kuona majenzi yake ya hapo awali yalianza kuharibika", akaongeza kueleza.**

Alimaliza maelezo yake kwa kusema kuwa kuanza kwa majenzi ya msikiti huo sio kukamilika kwake lakini kutakamilika pekee ikiwa wananchi watasaidia na kujitolea kwa moyo wa *NYAYO* wa Upendo, Amani na Umoja wa wananchi wa tabaka zote.

Mbali na mwaliko kwa Bw. Nassir na Mkuu wa Mkoa, Bw. Haji, watayarishi wa Harambee hiyo pia wamewaalika viongozi mbali mbali kuhudhuria na kujumuika na wananchi siku hiyo ya Novemba 10, kuchangia pesa za kukamilisha jengo hilo la Msikiti wa Shakombo.

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

Wasafishaji mashuhuri wa picha za rangi za *FUJI* ulimwenguni sasa wanapatkiana njini Mombasa

*Aina zote za picha za rangi zinachapishwa:*
*FUJI • KODAK • AGFA SAKURA • COLOURAMA*

*KWA USAFISHAJI WA PICHA ZAKO ZOTE ZA RANGI HAKIKISHA UNAZITUMA KWA MITAMBO MIPYA YA KISASAS YA FUJI*

Zungumza na *Riaz Alibhai* kwa simu 313589, Mombasa ama fika kwenye mitambo hiyo mipya ya *FUJI*, iliyo pakana na afisi ya *Coastweek*, gorofa ya kwanza ya jumba la Banki ya Grindlays, katika barabara ya Digo Road na Nkrumah road.

FUJI FUJI FUJI FUJI FUJI

# Kijana Khalid Asifika Kwa Utayarishi Na Utengenezaji Wa 'Maziwa Lala'

na Abdulrahman Sheriff

**UNAPOTEMBELEA popote mjini Lamu, ukianzia Mkomani, Ukipitia Mtamwini, Riyadha, Langoni na hata Shell ukiuliza jina la "Yoghurt Inn" hakuna atakayekosa kukufahamisha kwani ni hoteli iliyo maarufu sana yenyi makao yake huko Mkomani.**

**Maana hasa ya neno *"Yoghurt"* ni Maziwa Lala ama Maziwa ya Kuganda. Basi umaarufu wake huo umetokana na hoteli hiyo kuuza maziwa lala yenye ladha tamu na inayowapendeza wenye kunywa. Hiyo ni hoteli mpay yenye umri usiozidi miaka miwili.**

**Hoteli hiyo inamilikiwa na kijana mwingine ambaye amejitolea mhanga kuona habaki nyuma katika kazi ya kuendesha biashara hiyo. Kijana huyo ni Khalid Ahmed Ali, mwenye umri wa miaka 25, umri ambao hutokubali kama anaweza kuendesha kazi vyema.**

**Lakini kijana Khalid Ahmed Ali amewadhihirishia watu kwamba anaweza kuonyesha mfano kwa vijana wenzake. Mbali na hayo Maziwa Lala, hoteli hiyo inauza vyakula kadha maarufu vikiwemo vile vya aina ambazo wageni kutoka kila pembe ya dunia huvitumia.**

**Kijana Khalid husimamia mwenyewe mapishi ya vyakula kutoka Ujerumani (German), Italia (Italy), Amerika (U.S.A.), Ufaransa (France), Swizerland na uingereza. Siku ya Ijumaa hoteli hiyo hufungwa kwa ajili ya kuwapa nafasi wafanyakazi mapumziko na pia waweze kufanya Ibada zao; kama ilivyo desturi ya watu wa mji huo.**

## SERANI

**Khalid alianza kusoma katika Shule ya Serani Primary School ya Mombasa na akamaliza masoma ya Msingi mnamo 1974. Baadaye akachukuwa masomo ya *"Book-Keeping"* na *"Accounts"* kwa muda wa mwaka mmoja. Miaka miwili baadaye, akarudi Lamu na kutumikia hoteli ya babake iliyokuwa ikijulikana kama Tajaribu.**

**Hoteli ya Tajaribu ilifanyiwa marekebisho mnamo mwaka 1982 ambapo Khalid alishikilia usukani hadi mwaka jana alipoamua kulibadilisha jina na kuita "Yoghurt Inn" kwa ajili ya umaarufu wa Maziwa Lala yanayotengezwa hapo. Yeye mwenyewe ndiye Mwalimu na wa mjuzi kutengeneza Maziwa Lala hayo.**

## DINI

**Kijana Khalid hakubaki nyuma katika kutimiza lengo la wajibu wa dini yake na akaamua kuoa. Amemuoa Mwanamke wa Kiamerika ambaye amesilimu na kwa wakati huu ana mtoto mmoja wa kiume. Amesema vyakula vyuzwavo hapo ni pamoja na Kamba, Supuna vyakula maalum vya aina mbali mbali.**

**Khalid ameniambia kwamba hatachoka kuvumbua aina nyingine za vyakula ambavyo vitawapendeza wananchi. Hakika Khalid na mwenzake Abdallah Mohammed Said Bathawab (stori ilitokea COASTWEEK 11-17/10/85) wameonyesha mfano ambao unastahili kuigwa na vij. na wenzao kwenye harakati za kujipatia maisha bora.**

Farucci

BINT EL SUDAN
Perfume • Powder
Pomade • Deodorant

MARASHI
ASILI YA MAPENZI
HAKIKA
UTA FURAHI

## JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA 'BINT EL SUDAN - GIFT PACK' KWA MSHINDI WA PILI NA WATATU ATAPATA ZAWADI YA FLANA YA FARUCCI

## CROSSWORD No. 220

*KWENDA KULIA:*

1. Aina ya samaki wa maji ya baridi. 5. Neno la kukanusha, hapana. 6. Zamani ikiitwa mvita. 9. Nusu ya Dada. 10. Komosha vita. 11. Hisia apatayo mtu anapokula kama embe bichi. 13. Mashtaka, daawa. 14. Mguu mkubwa. 16. Ubinadamu. 18. Kinyume cha PM. 19. Sila ya kupigia ndege. 21. Mfuko wa kisu. 22. Shika amri.

*KWENDA CHINI:*

1. Tufani, Dhoruba. 2. Ufupi wa baba yake, 3. Kitu cha madini hutumika kama silaha hatari. 4. Matunda ya mbibo. 7. Mtu mwenye tabia ya kutaka kujua habari za watu. 8. Baba mdogo. 12. Kontinenti moja la dunia. 15. Chombo cha kulia chakula. 16. Wa kufukizia. 17. Ni Kivazi kisha ni ndege. 19. Kiungo cha maneno. 20. NT haigeuki.

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 219**

*KWENDA KULIA:* 1. MNYAPARA, 6. UANI, 8. KALA, 9. GAE, 11. AMINA, 13. HUA, 15. ZA, 16. KANU, 17. ISHE, 18. TEUA, 19. SAKAMA. *KWENDA CHINI:* 1. MKUNAZI, 2. YUNGI, 3.PO, 4. RIADHA, 5. KAMAU, 7. IANZE, 10. EA, 12. MASHA, 14. UNGUA, 16. KUTA.

**WASHINDI WA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 219**

1. ESHA A. NASSIR, Sanduku La Posta, 98739, Mombasa. 2. HARRISON KATANA, Sanduku La Posta 87294, Mombasa. 3. MISS RUTH J. MUNGA Sanduku La Posta 84184, MOMBASA.

**Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:—**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Kila baada ya wiki mbili, Mshindi wa kwanza atapata viatu maridadi vya Farucci; wa pili atapata 'Bint El-Sudan-Gift Pack' na watatu atajinyakulia flana ya Farucci. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa. Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Mhariri COASTWEEK, S. L. P. 87270, Mombasa. Mwisho wa kutuma Majibu na jumatano, **October 30, 1985** saa, nne asubuhi.




**JINA**..............................

**SANDUKU LA POSTA**..............................

..............................

# SIKUKUU YA KENYATTA DEI

**WAZIRI Mdogo wa Ardhi na Makao, Bw. Sheriff Nassir aliye pia Mwenyekiti wa KANU wilayani Mombasa na Mbunge wa Mombasa ya Kati anaonekana wakati wa dansi ya kusherehekea Sikukuu ya Kenyatta Dei iliyofanyika katika Hoteli ya Oceanic.**

PICHA: LAWRENCE MWANTHI